# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 10: "Siku ya Mapatano"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA/THELMA MWADZAYA**

**List of characters for episode 10:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Layton-Browne (Philip's father), male (50)
- Harry, male (17)
- Layla, female (16)
- Roshi, female (16)
- Mat, male (17)
- Ishmail Omer (Laylas father), male (43)
- Chief Dembele (Harry's father), male (51)
- Father Barnabus ( Harry's uncle), male (49)
- Mrs. Milulu (School Director), female (48)
- Sister Rebecca, female (28)
- Hassan, male (12)

- <u>+ Students</u>
- <u>+ Linesman (at sports competition)</u>

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya kumi na ya mwisho kwenye mfululizo wa mchezo wa Redio ''DARAJA LA GORI''. Hii ni hadithi ya kusikitisha inayoelezea jinsi siasa na Dini zinavyoweza kutumiwa kuleta migogoro baina ya Jamii mbili, familia na hata vijana wawili Harry na Layla wanaolazimika kulificha Penzi lao.Katika makala hii ya mwisho ya'Siku ya Mapatano'' Harry na Layla wanazifahamisha familia zao kuhusu mipango yao ya baadaye. Je Familia hizi zitalichukuliaje suala hili?Kwanza kabisa tega sikio kwani Babake Philip hatimaye anamfichualia siri yake mwanawe. Philip ni rafiki mkubwa wa Harry na anasimulia.**

**3. PHILIP/NARRATOR:** **Nikiitathmini miaka miwili iliyopita, naona kuwa nilichagizwana wivu…nilimuone Harry wivu.Kila dini inaupinga wivu nayo misingi ya Ubuntu nayo pia inaupiga vita.Yote yalidhihirika pale Baba aliponifichulia siri aliyokuwa nayo kwa miaka mingi.**

**Scene 1. At the Layton-Browne's**

**Layton-Browne, Philip**

**4. SFX: soft music (radio)**

**5. P'S FATHER:** ***(feeling uneasy)*** **Philip, haya yaliyotokea kitambo kabla hata hujazaliwa.**

**6. PHILIP:** **Nini kilichotokea Baba?**

**7. P's FATHER:** **(remembering) Mwanamke kwenye ile picha iliyo mezani kwangu alikuwa mkaguzi wa hesabu. Idara yetu ya fedha ilikumbwa na visa vingi vya**

**udanganyifu na Mwanamke huyu aliagizwa kuzikagua takwimu zetu.Shughuli hiyo ilichukua muda wa siku kadhaa.Alikuwa akifanya kazi mpaka jioni sasa kila siku…na tulipata fursa ya kujuana…..**

**8. PHILIP:** **(irritated) OK, Kwa hivyo alikuwa mpenzi wako kabla ya kutengana?Na bado unampenda sivyo?**

**9. P's FATHER:** **Ndio…ummm ila si hivyo unavyosema… tulipendana sana…ila alikuwa muislamu na ijapokuwa familia yetu haikuwa ikifuatilia dini kwa karibu…tuliwekewa vikwazo.**

**10. PHILIP:** **Na kisha baadaye ikawaje? Na alikuwa ni nani hasa? Mbona hutaki kunieleza baba?**

**11. P's FATHER:** ***(reluctantly)*** **Aliitwa… aliitwa Anisa.**

**12. PHILIP:** **Anisa?**

**13. P'S FATHER:** **Ulimfahamu kama Bi Omer wakati wa uhai wake**

**14. PHILIP:** ***(gasps)*** **Bi Omer? Yaani una… unamanisha… Mamake Layla? Baba! Na huyo mtoto aliyembeba pichani? Usiniambie ni…. tafadhali usiniambie ni…....**

**Cut ambience. Fade music** ***(upset)***

**15. PHILIP/NARRATOR: Hatimaye maswali mengi niliyokuwa nayo sasa yalikuwa yamenza kupata majibu.Layla alinivutia kwasababu alikuwa ndugu yangu kwa baba! Mamake aliolewa na Mzee Omer alipokuwa na mimba changa ya Layla, lakini Mzee Omer hakulijua hilo. Baadaye akamzaa mtoto wa kiume Hassan,lakini hakumwambia ukweli kumhusu Layla na alipofariki alizikwa na siri zake….Hatimaye nikawa nimejua! .** ***(sounding more cheerful)*** **Lakini kwa upande mwengine, shule ya Ubuntu inasherehekea siku ya Mapatano inayowaleta pamoja wakaazi wote wa mji wa Gori!**

**16. <u>FADE UP NOISE OF CELEBRATIONS</u>**

**Scene 2. Outside Reunion Centre**

**Harry, Layla, Mat, Philip, Roshi, Mr Omer, Chief Dembele, Father B, Sister Rebecca, Hassan, students, linesman**

17. **SFX: Outside Reunion Centre, cheering students, festive music**

18. **MAT:** *(shouting over the noise)* **Philip! usikae peke yako ukiwaza hapo..!. Njoo tusherehekee pamoja…, tumeshinda kikombe cha mjadala! Njoo tusherehekee!**

19. **HARRY:** **Ni kweli Mat.., Philip… chukua hiyo Kamera utupige picha ya ukumbusho wa madume watatu wa chuo cha Ubuntu…Tayari………** ***(laughing)*** **Tatu…mbili… moja….**

20. **ALL:** **(shouting) CHEESE!**

21. **SFX: camera clicks**

22. **HARRY:** **Sawa kabisa…! Na wewe njoo hapa Philip, tunataka uwapige picha Roshi na Layla wakishinda mbio za mita 400 kuruka vihunzi!**

**23. PHILIP:** **Sawa, Harry! Lakini baadhi ya Waislamu hawapendi kupigwa picha, lazima kwanza niwaombe ruhusa.**

**24. HARRY:** **Ni Sawa, Bi Milulu aliwauliza na wote wakaridhia kupigwa picha zitakazochapishwa kwenye gazeti la Chuo na hata Gazeti la Babako.**

**25. PHILIP:** **Napenda mavazi yao ya mikono mirefu, suruali za wasichana hawa wa Kiislamu, bila kusahau kitambara cha kichwa - lazima nisongee karibu zaidi.**

**26. HARRY:** **Tazama Mat! Hata wavulana pia wamevalia mavazi yanayoifunika miili yao.Nimearifiwa kuwa ni mavazi maalum na mepesi ambayo huwasaidia kutosikia joto.**

**27. MAT:** **Tumefanikiwa,sasa kila anayetaka anaweza kushiriki!**

***28.*** **LINESMAN: (distant shout)** ***"On your marks……Go!"***

**29. <u>SFX: RUNNING/WHISTLING/CHEERING</u>**

**30. SINGING UBUNTU ANTHEM ABOVE THE CHEERING.**

**OFF MIC**

**31. HASSAN:** *(shouting, excited)* Kimbia! **…, Kazana! Layla…. Kazana !**

**32. MR OMER:** *(excited)* **Kazana … ongeza mwendo ndio….hasa… Huyo binti yangu! Bado yuko nafasi ya tatu! Tazama Hassan, yule pale Dada Rebecca kutoka Hospitalini!!**

**33. REBECCA:** **Oh, Habari Hassan. Habari Bw Omer!... ohh na sasa ameanza kuwashinda, … ndio kaza mwendo Layla!**

*34.* **HASSAN:** **Sasa Roshi ni wa pili,… Layla anaongoza!...!** ***HOORAY!***

**35. SFX: Roshi and Layla panting heavily**

**ON MIC**

**36. ALL:** **Hongereni sana wasichana**!

**37. ROSHI:** *(panting)Hongera* **Layla, umetusaidia sana kushinda kikombe!. Philip tupige picha**!

**38. PHILIP:** **Bila shaka.., sasa tabasamu !**

**39. SFX: camera clicks**

**40. PHILIP:** **Ahsante!**

**41. LAYLA:** *(panting)* **Ahsante, Philip!, hebu nione.. Ahh ni nzuri!!**

**42. PHILIP:** **Nitakupa nakala, kama ukumbusho….**

**43. LAYLA:** **Ahsante sana Philip, unavyozungumza ni kama zawadi ya kuagana!**

**44. PHILIP:** *(awkwardly)* **Tunaweza kusema hivyo… unajua… ehh nilitaka kusema….!...**

**45. LAYLA:** *(interrupting)* **Ohhh Harry, Babako na Kasisi wanazungumza na Babangu. Hebu twende.. Tuonane baadaye Philip!**

**46. PHILIP/NARRATOR: Niliamua kutomueleza Layla yote ninayofahamu- kuhusu uhusiano wa mamake na Babangu- na udugu wetu. Nilihitaji muda kidogo tu kuwa naye kama Dadangu!! Lakini alikuwa ameshikwa na msisimko mkubwa alipoziona Familia ya Omer na Dembele hatimaye zikiwa pamoja!. Hivyo nikamruhusu aende, kwani nilifahamu kwamba hili lilikuwa tukio la Kihistoria.**

**47. HARRY: Bw Omer,Baba na Askofu Babangu mdogo**!

**48. FATHER B: Hujambo Harry**- ***(stops suddenly)*****Askofu nani?**

**49. HARRY: Samahani**, **Baba mdogo Barnabus! Hilo ni jina la Utani nimekupa.!**

**50. ALL: (Everyone laughs)**

**51. MR OMER: Layla, Binti yangu,…. Hongera umefanya vizuri sana!**

**52. HASSAN:** **Hongera Dada! Sister Rebbecca yuko pale na Binti yake Abigali. Amesema tutakapotimiza umri wa miaka 16, sote tutajiunga na Chuo Cha Ubuntu. Na Baba ameridhia!**

**53. LAYLA:** **Habari njema sana! *(hesitantly)* Na… uh…Unafahamu kwamba wao ni wayahudi sivyo?**

**54. HASSAN:** **Walemba kwa taarifa yako!. Mimi na yeye tumekuwa tukilinganisha mafundisho ya kitabu kitakatifu cha wayahudi Torah, na kile cha Waislamu Qur'an. Ningependa kusomea Historia ya dini wakati nikuwa mkubwa!**

**55. LAYLA:** **Hebu nikukumbatie mdogo wangu. Nimefurahi kuyasikia hayo**!

**56. HASSAN:** **Kwanini! Mimi sikushinda mbio za mita 400,ni wewe!**

**57. LAYLA:** **Lakini wewe pia umeshinda kwani umeruka viunzi vingi zaidi Hassan. Vikwazo vilivyotenganisha familia yetu na ile ya jirani. Umekipa sifa Chuo cha Ubuntu**!

**58. HARRY:** ***(breathing in deeply, moved)*** **Baba mimi na Layla tunataka……**

**59. LAYLA:** ***(interrupting, excited)*** **Chifu Dembele, na Baba!... Mimi na Harry tunataka kuweka mapenzi yetu hadharani.**

**60. CHIEF DEMBELE:** **Ohhh! Jambo geni sana katika tamaduni yetu.. Msichana anamuomba mvulana awe mpenzi wake!Kweli huu ni ulimwengu wa kisasa.!(laughs) Lakini katika utamaduni wetu, lazima tulete Ng'ombe kwa Babako ili awabariki.**

**61. LAYLA:** **Oh hilo ni jambo la kufurahisha sana!!**

**62. MR OMER:** **Namuelewa Chifu Dembele na pia naliheshimu wazo hilo.Tuna matambiko yanayofanana katika jamii zetu, lakini kwanza ni lazima tukae tuzungumze ili tuweze kuzifahamu vyema tamaduni zetu. Harry siwezi kukulazimisha kufuata tamaduni au dini yetu. Wewe na Layla mtajiunga na chuo kikuu kilicho mbali kabisa na sisi, ambako hatutaweza kuwazuwia. Hivyo basi nataka mukiwa huko muheshimiane. Tafadhali umuheshimu Binti yangu, na kumbuka sio wewe pekee unayempenda! Kwa hivyo musaidiane.**

**63. FATHER B:** **Tunaweza kushirikiana na kutangamana na wakti huo huo kuhifadhi tamaduni zetu.Siasa ndizo zinazoingilia kati na aghalabu tunatumia tofauti za kidini kufikia malengo yetu.Hilo si sahihi kabisa. Nililitambua hilo niliposikia kuwa Mchungaji Henry Immanuel alitoweka na pesa za waumini wake.Bw Omer- mimi kama mwanachama wa Baraza la Maendeleo ya Mji, nadhani tuna mengi yanayotuleta pamoja**

**ukilinganisha na waumini wengine wa dini yangu!**

**64. CHIEF DEMBELE: Umesema vizuri Kakangu! Tunachohitaji zaidi ni kuiimarisha uchumi na masuala ya jamii yote! Huo ndio Ubuntu.Hilo ndilo linalotuunganisha!.**

**65. MR OMER: Ni kweli kabisa! Na ili kusherehekea habari hizi njema, ningependa kuwaalika nyote nyumbani kwangu! Hata wewe Sister Rebecca na Binti yako Abigali: Najivuna sana kuwa miongoni mwenu. Nimefurahishwa sana na kazi yako. Maana umeyaokoa maisha ya mwanangu alipojiteketeza!**

**66. REBECCA: Ahsante sana Bw Omer, Hassan alitaka kuokolewa. Kama ujuavyo hakuna Mtu aliyechagua kuzaliwa Afrika, Myahudi au Mkristo- sote tulikuja hapa ulimwenguni pasi na kufahamu, na tunategemeana ili kuishi kwa amani.**

**67. ALL: (<u>Laughing, kissing, murmurs of agreement)</u>**

**68. BRIDGING MUSIC**

**69. PHILIP/NARRATOR: Muhula wa kwanza ulikuwa unaelekea kumalizika katika shule ya Ubuntu. Tayari tumemaliza miaka miwili pamoja lakini Mwaka uliotangulia daima nitaukumbuka, kwani ulinifunza mengi kufika hali niliyo kwa hivi sasa, kwani sasa naishi maisha mazuri, bila ya wivu au chuki. Kwa hakika hali hii imebadilisha maisha yangu kimawazo na hata kiafya.Pia Hassan alikuwa amejifunza mengi sana. Na kama adhabu ya jaribio la kuteketeza kanisa hilo, yeye na wavulana wengine katika chuo cha Madrassa walihitajika kusaidia katika ujenzi wa kituo cha utamaduni cha Mapatano. Na sasa kila mmoja anafurahia kukitembelea kituo hicho pamoja na kushiriki michezoni kama washiriki wa timu moja!Lakini subiri kwanza – Harry ananiita……**

| | | |
|---|---|---|
| **70.** | **HARRY:** | ***(off mic)*** **Philip…!** ***(on mic)*** **Philip –kabla ya kuondoka tafadhali tupige picha moja hapa!** |
| **71.** | **LAYLA:** | **Tafadhali Philip, picha ya ukumbusho!** |
| **72.** | **PHILIP:** | **Sawa…! Mnataka kupiga wapi?** |
| **73.** | **LAYLA:** | **Katika Daraja la mto Gori!** |
| **74.** | **PHILIP:** | **Wewe na Harry! Katika daraja la Mto Gori?** |
| **75.** | **HARRY/LAYLA:** | **Naam Phil** ***(laughing)*****, Katika daraja hilo la Mto Gori! Hatuhitaji tena kujificha chini ya Daraja!** |
| ***76.*** | **ALL:** | ***(All laughing)*** |

**77.** <u>**SIG TUNE UP**</u>

## 78. OUTRO:

**Hadi hapo tunafika mwisho wa sehemu ya kumi na ya mwisho ya mfululizo wa mchezo huu wa Redio DARAJA LA MTO GORI. Hadithi iliyoandikwa na Romie Singh. Penzi la Harry na Layla lilikuwa thabiti kushinda migogoro uliodumu kwa karne moja baina ya Familia hizo mbili. Majadiliano, ushirikiano na kuvumiliana licha ya tofauti za imani, ndio msingi wa kurejesha amani na maelewano** katika mji wa Gori..

Kumbuka ukiwa na maoni au ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki, Tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine Kwaheri kwa sasa.

**END OF EPISODE 10**